06 June 2025

# Kituo cha malalamiko cha kutoa taarifana malalamiko

**Kituo cha malalamiko cha Finnfund kinaweza kutumika kuripoti kwa siri kuhusu utovu wa nidhamu unaoshukiwa kutokea, makosa makubwa yanayoathiri watu au wajibu wetu wa kimazingira na kijamii, au ukiukaji mwingine wa sera, kanuni au miongozo inayoongoza shughuli za Finnfund.**

Tunajitahidi kukuza uwazi na maadili katika shughuli zetu zote. Kwa hivyo tunawahimiza wadau wetu wote kutumia mfumo wetu wa kutuma malalamiko kuhusu utovu wa nidhamu wowote unaoshukiwa, ukiukaji mkubwa wa uwajibikiaji wa mazingira na kijamii na haki za binadamu, au ukiukaji mwingine wa sera, kanuni au miongozo inayoongoza shughuli za Finnfund ambayo inaweza kuibuka kuhusiana na shughuli za Finnfund au makampuni yanayofadhiliwa na Finnfund, ili yaweze kushughulikiwa ipasavyo. Hatua hii pia ni muhimu kwa maendeleo ya shughuli zetu.

**Katika ukurasa huu, tutaeleza zaidi kuhusu mfumo wa kutuma malalamiko, jinsi unavyoweza kuwasilisha ripoti, na jinsi Finnfund inavyochakata ripoti inazopokea.**

**Maudhui yaliyomo kwenye ukurasa huu (tafadhali angalia viungo hapa chini) na mfumo wa kuripoti yanapatikana katika lugha zifuatazo: Kiingereza, Kifini, Kifaransa, Kihispania, Kireno na Kiswahili. Ujumbe katika lugha yoyote unaweza kutumwa kupitia huduma ya simu.**

- .Ilmoita väärinkäytösepäilystä (Finnish)
- Complaints channel for whistleblowing and grievances (français, pdf)
- Canal de quejas y denuncias (español, pdf)
- Canal de denúncias e reclamações (português, pdf)
- Kituo cha malalamiko kwa ufichuzi na malalamiko (swahili, pdf)

### Je, Mfumo wa kutuma malalamiko unategemea nini?

Mfumo wa kutuma malalamiko wa Finnfund na miongozo na taratibu zinazohusiana zinatokanana yafuatayo:

- Sheria ya Jumla ya Ulinzi wa Data ya Umoja wa Ulaya (EU 679/2016)
- Maelekezo ya Umoja wa Ulaya kuhusu Kutuma Ripoti (EU 2019/1937)
- Sheria ya Ulinzi wa Watumaji Ripoti (1171/2022)
- Sheria ya Kuzuia Uchapishaji Pesa Haramu na Ufadhili wa Kigaidi (444/2017)
- Kanuni za maadili na uwajibikaji za Finnfund, kama vile Kanuni Elekezi za Umoja wa Mataifa kuhusu Biashara na Haki za Kibinadamu (UNGP) zilizotajwa katika sera ya haki za binadamu na mbinu ya haki za binadamu ya Finland (HRBA)

Wigo wa mfumo wa kutuma malalamiko wa Finnfund ni pana kuliko ilivyobainishwa kwa mifumo ya kuripoti katika sheria za Kifini. Mbali na ulinzi wa watoa taarifa unaotolewa katika sheria za Kifini, **Finnfund hujitahidi katika hali zote kulinda faragha na usalama wa watoa taarifa**.

### Je, mfumo wa kutuma malalamiko unahusu nini?

Mfumo wa kutuma malalamiko wa Finnfund unaweza kutumika kuripoti kuhusu utovu wa nidhamu unaoshukiwa kutokea, makosa makubwa yanayoathiri watu au wajibu wetu wa kimazingira na kijamii, au ukiukaji mwingine wa sera, kanuni au miongozo inayoongoza shughuli za Finnfund. Kwa hivyo, mfumo wa kutuma malalamiko unaweza kutumika kuripoti ukiukaji wa kanuni zilizowekwa katika sheria ya ulinzi wa watumaji ripoti pamoja na kanuni za uwajibikaji za Finnfund na sera nyinginezo.

Kwa kuripoti, unaweza kusaidia Finnfund kuchukua hatua mapema kuhusu utovu wa nidhamu na ukiukaji unaoweza kutokea.

Finnfund pia inawahitaji wawekezaji wake kuanzisha na kudumisha mifumo ya kutuma malalamiko inayoweza kufikiwa na watu wote.

Tafadhali kumbuka kwamba Finnfund pia ina fomu ya mawasiliano ya kupokea maoni ya wateja na mawasiliano mengine ya kawaida, inayopatikana kwenye anwani: **www.finnfund.fi/otayhteyttä.**

**Je, ripoti inaweza kuwasilishwa kwa misingi gani?**

Mtumaji ripoti hahitaji kuwa na uthibitisho wa utovu wa nidhamu au ukiukaji kabla ya kuwasilisha ripoti, lakini ni lazima awe na sababu zinazokubalika za kuamini kwamba taarifa zilizo katika ripoti ni sahihi. Ripoti zote zinapaswa kuwasilishwa kwa uaminifu na nia njema. Ni marufuku kutuma ripoti hasidi au isiyo sahihi makusudi. Mtuma ripoti ambaye hutoa au kufichua habari za uwongo kwa makusudi katika ripoti, anaweza kutozwa faini kwa kukiuka sheria ya ulinzi wa watuma ripoti.

(VISANDUKU KUNJUZI)

**1 Kuwasilisha ripoti**

Mtu yeyote anaweza kututumia ujumbe, bila kujitambulisha au pia akiambataisha maelezo yake ya binafsi. Mfumo huu unatoa mbinu mbili za msingi za kuripoti:

- Ukiukaji wote unaoshukiwa unaweza kuripotiwa kwa kutuma ujumbe wa siri au bila kujitambilisha kwa maandishi au ujumbe wa sauti kwenye anwani : https://report.whistleb.com/fi/finnfund

- Vinginevyo, ripoti inaweza pia kutumwa kwa njia ya posta kwa Teollisen yhteistyön rahasto Oy (Finnfund), Timu ya Malalamiko, SLP 147, 00181 Helsinki, Finland

Ikiwa mfanyakazi wa Finnfund anataka kuripoti ukiukaji unaoshukiwa unaohusisha Finnfund au mmoja wa wafanyakazi wake, tunapendekeza kwamba suala hilo liripotiwe kwanza kabisa kwa mkuu wa karibu wa mfanyakazi husika. Mfanyakazi wa Finnfund akipenda, au ikiwa tuhuma inahusu mkuu wake, suala hilo linaweza pia kuripotiwa kwa msimamizi wa msimamizi wake au kwa idara ya rasilimali watu ya Finnfund:people-culture@finnfund.fi

Iwapo mtumaji ripoti ni mfanyakazi wa kampuni inayofadhiliwa na Finnfund au mshikadau mwingine, tunapendekeza kwamba ripoti ifanywe hasa kupitia njia za kuripoti za kampuni hiyo. Finnfund inaagiza kwamba kampuni inazofadhili ziwe na mfumo wa kutuma malalamiko kwa wafanyakazi wao wenyewe na washikadau wa nje. Ikiwa ripoti inahusu kampuni inayofadhiliwa na Finnfund, mtumaji ripoti anaweza pia kuchagua kuripoti suala hilo kibinafsi kwa mfanyakazi wa Finnfund, ambaye atarekodi ripoti hiyo na kuituma kama ilivyo kwa timu ya uchunguzi kwa ajili ya kuchakatwa.

**Ripoti zote zilizopokelewa zitashughulikiwa kwa usiri, licha ya mbinu ya kuripoti iliyotumika.**

**Ripoti isiyomtambulisha aliyeituma**

Iwapo mtumaji ripoti angependa kutojitambua, anaweza kuwasilisha ripoti bila kujitambulisha. Mfumo wa kutuma malalamiko unasimamiwa na kampuni mtoa huduma wa nje inayoitwa WhistleB. Mfumo wa kutuma malalamiko hulinda utambulisho kwa kuondoa maelezo kama vile anwani za IP ambazo zinaweza kufichua utambulisho wa mtumaji ripoti. Mtu anayewasilisha ripoti hiyo pia hatatambuliwa katika majadiliano yoyote zaidi yanayowahusisha watu wanaoshughulikia kesi hiyo. Arifa zote husimbwa kwa njia fiche.

Ni vyema kufahamu kwamba kuripoti bila kujitambulisha kunaweza kuzuia uchunguzi, ndiyo maana watumaji ripoti wanahimizwa kufichua utambulisho wao kwa uwazi. Ili utovu wa nidhamu au ukiukaji

unaoshukiwa uchunguzwe ipasavyo, **suala hilo linafaa kufafanuliwa kwa kina iwezekanavyo katika ripoti**. Ni muhimu kukumbuka pia kwamba hata kama mtumaji ripoti hajawasilisha jina na maelezo yake ya mawasiliano, utambulisho wake bado unaweza kufichuliwa kulingana na maelezo yaliyotolewa wakati wa uchunguzi wa kina wa kesi hiyo.

**MUHIMU: Kumbuka kuhifadhi nenosiri na jina lako la mtumiaji**

Baada ya ripoti kuwasilishwa kwa kituo cha kufichua, mtumaji malalamiko atapewa nenosiri na jina la mtumiaji kiotomatiki. Nenosiri na jina hili la mtumiaji litahitajika katika siku zijazo ili kuingia kwenye mfumo wa kutuma malalamiko, jambo ambalo linahitajika na ni muhimu pia ikiwa mtumaji ripoti anataka kushiriki katika majadiliano, kutoa maelezo ya ziada, au kusikia kuhusu matokeo ya uchunguzi baadaye. Kutoa maelezo ya ziada mara nyingi ni muhimu kwa ajili ya uchakataji wa suala husika pia**. Kwa hivyo ni muhimu kwamba mtumaji ripoti ahifadhi jina la mtumiaji na nenosiri, kisha kuingia tena kwenye mfumo ili kuendelea na majadiliano. Nenosiri haliwezi kuwekwa upya.** Nenosiri likipotea, mtumaji ripoti anaweza kuhitaji kuwasilisha tena ripoti hiyo.

Ripoti zote zilizopokewa, pamoja na mawasiliano yao husika yatarekodiwa katika mfumo wa kutuma malalamiko, ambayo yanaweza kufikiwa na timu ya uchunguzi ya Finnfund pekee. Mazungumzo yote yanayomhusisha mtumaji ripoti yatafanyika kwa kutumia njia ya mawasiliano iliyochaguliwa na mtumaji ripoti. Kuwasiliana kwa barua ya posta kunawezekana tu ikiwa ripoti inajumuisha maelezo ya mawasiliano ya mtumaji ripoti yanayowezesha barua ya posta kutumwa.

Ikiwa ripoti imewasilishwa kwenye mfumo wa kutuma malalamiko wa Finnfund, mtumaji ripoti atapokea uthibitisho wa kupokelewa ndani ya siku saba (7). Ujumbe huu unaweza kusomwa katika mfumo wa kutuma malalamiko. Ikiwa mtumaji ripoti amewasilisha anwani yake ya barua pepe, pia atapokea ujumbe kwa barua pepe. Ikiwa ripoti imetumwa kwa barua au kuwasilishwa na mtu binafsi kwa mfanyakazi wa Finnfund, Finnfund itafuata kanuni yake ya kutotuma uthibitisho tofauti wa kupokea.

**Mifumo ya upili**

Mbinu zilizo hapa juu ndizo njia zinazopendekezwa za kutuma ripoti. Tuhuma za utovu wa nidhamu zinazohusiana na wigo wa utekelezaji Sheria ya Ulinzi ya mtumaji malalamiko zinaweza kuripotiwa kwa upili kwa mamlaka husika kupitia njia ya nje ya upeperushaji inayodumishwa na Chansela wa Haki:https://oikeuskansleri.fi/miten-ilmoitus-tehdaan.

Tuhuma za utovu wa nidhamu ambazo haziko chini ya wigo wa Sheria ya Ulinzi ya mtumaji ripoti iliyotajwa hapa juu zinaweza kuripotiwa kwa njia ya upili kwa OECD National Contact Point nchini Ufini:finland.tem@gov.fi.

## 2 Uchunguzi na kutuma taarifa kuhusu uamuzi

Timu ya uchunguzi itamjulisha mtumaji ripoti ndani ya muda usiozidi miezi mitatu (3) baada ya kutuma uthibitisho wa kupokea kesi iwapo ripoti hiyo itachunguzwa, na hatua zitakazochukuliwa kwa misingi ya ripoti hiyo.

Wakati wa uchunguzi, timu ya uchunguzi itauliza maswali zaidi inapohitajika na kujadili hoja na mtumaji ripoti kwa kutumia mfumo uliochaguliwa na mtumaji ripoti. Matokeo ya uchunguzi pia yatawasilishwa kwa mtumaji ripoti kupitia mfumo aliouchagua. Ikiwa ripoti iliwasilishwa kupitia mfumo wa kutuma malalamiko, ni muhimu pia kwamba mtumaji ripoti ahifadhi nenosiri na jina lake la mtumiaji na atumie maelezo haya kuingia tena kwenye mfumo, ikiwa angependa kuendelea na mjadala na kusikia kuhusu matokeo ya uchunguzi.

Iwapo matokeo ya uchunguzi yanaweza kuathiri haki, maslahi, au wajibu wa mada ya ripoti au wahusika wengine, timu ya uchunguzi italazimika, inapowezekana, kuripoti matokeo ya uchunguzi kwao pia.

Kanuni zifuatazo zitazingatiwa katika uchunguzi wa kesi:

- **Ripoti zote huchukuliwa kwa uzito na kushughulikiwa kwa usiri na bila upendeleo.**

- Uchunguzi utaanzishwa ikiwa kuna sababu za kuridhisha za kushuku kwamba utovu wa nidhamu, ukiukaji mkubwa wa uwajibikaji wa kimazingira na kijamii au haki za binadamu, au ukiukaji mwingine wa sera, miongozo au maagizo yanayoongoza shughuli za Finnfund ambao ni mbaya kuliko tuhuma au kutoridhika kwa ujumla.

- Uchunguzi utafanywa na timu ya uchunguzi ya Finnfund. Timu ya uchunguzi inaweza, kwa msingi wa tukio baada ya tukio, kutumia wataalam wa Finnfund wenyewe au wa nje na kushiriki habari kwa wafadhili wengine, hata hivyo, inapaswa kuhakikisha wakati wote kwamba kanuni za ulinzi wa watoa taarifa, uhuru, na ulinzi wa data zimezingatiwa. Watu ambao wanashukiwa au wanaohusishwa na utovu wa nidhamu au ukiukaji hawatashiriki katika uchunguzi wa ripoti unaoshukiwa hawatashiriki katika uchunguzi wa ripoti husika.
-

Hakuna mwanachama wa timu ya uchunguzi au mtu mwingine yeyote anayehusika katika mchakato wa uchunguzi atajaribu kumtambua kwa njia yoyote ile mtumaji ripoti asiyejitambulisha.

(*Kumbuka: Katika muktadha huu, neno kutuma ripoti linarejelea utaratibu wa kuripoti uliowekwa katika Maagizo ya Kutuma Ripoti ya Umoja wa Ulaya na Sheria ya Ulinzi ya Mtumaji Ripoti ya Kifini. Neno malalamiko linamaanisha utaratibu wa kuripoti unaorejelewa katika sera ya haki za binadamu ya Finnfund na kanuni za uwajibikaji.)*

(MAANDISHI YA MSINGI YANAENDELEA)

**Mtumaji ripoti atalindwa vipi?**

Mtu yeyote anaweza kuripoti tuhuma zake bila hatari ya baadaye ya kuathiriwa, kubaguliwa, kulipiziwa kisasi au kuonewa. Hakika, hii inamaanisha kwamba sheria na masharti ya uhusiano wa ajira ya mtumaji ripoti anayeripoti tuhuma au wasiwasi halisi wa mujibu wa miongozo hii haitaathirika, na mtumaji ripoti hatakabiliwa na matokeo yoyote mabaya katika suala la ajira au haki za kimkataba, au kuathiriwa vinginevyo kwa sababu ya ripoti hii (hali inayojulikana kama marufuku ya kulipiza kisasi).

Finnfund haikubali vitisho vyovyote au aina nyingine za shinikizo au adhabu dhidi ya watoa taarifa, watetezi wa haki za binadamu au washikadau wengine. Mtumaji ripoti pia atalindwa ikiwa amefichua siri ya biashara katika ripoti yake, ili kulinda maslahi ya umma, au kuhusiana na ufichuaji wa taarifa zinazohusiana na ripoti hiyo.

Iwapo mtumaji ripoti atafichua au kuripoti habari kuhusu ukiukaji ambao umewekewa vikwazo au marufuku kwa makubaliano au kanuni, mtumaji ripoti hatawajibishwa isipokuwa kuchukua habari kunasababisha adhabu kwa mujibu wa sheria za Ufini. Sharti la ziada ni kwamba mtumaji ripoti lazima alikuwa na sababu za kuridhisha za kuamini wakati wa kuripoti kwamba kuripoti au kufichuliwa kwa maelezo kulihitajika ili kufichua ukiukaji huo.

Ulinzi wa mtumaji ripoti pia hutolewa kwa watu wanaomsaidia mtumaji ripoti katika utaratibu wa kuripoti, na watu wengine ambao wanahusiana na mtumaji ripoti na kutoa taarifa kuhusu kesi hiyo

.**Je, data ya kibinafsi inahifadhiwaje**?

Finnfund itahifadhi ripoti na data ya kibinafsi iliyomo, pamoja na hati za uchunguzi, katika kituo cha mtumaji ripoti kwa miaka mitano (5) kuanzia tarehe ya kupokelewa kwa ripoti hiyo. Ikiwa uhifadhi wa data ya kibinafsi inayohusiana na ripoti bado ni muhimu kwa madhumuni ya uchunguzi wa jinai, kesi za kisheria zinazosubiri, uchunguzi rasmi, au kulinda haki za mtumaji ripoti au mtu ambaye ni mhusika wa ripoti hiyo, hitaji la uhifadhi zaidi wa data litatathminiwa tena kabla ya miaka mitatu (3) baada ya uhakiki uliopita. Ukaguzi utarekodiwa katika mfumo wa kutuma malalamiko kama ingizo la sajili ya ripoti husika.

Data ya kibinafsi ambayo haihusiani bayana na uchakataji wa ripoti itafutwa bila uchelewashaji usiostahili.

## Je, haki za mwenye data ni gani?

Uchakataji wa data ya kibinafsi ya watumaji ripoti na watu wanaoripotiwa (wenye data) inategemea sheria ya ulinzi wa data inayotumika nchini Ufini wakati wowote.

Mwenye data ana haki ya kufikia data yake ya kibinafsi, kuomba kurekebishwa kwa data yake, kupinga uchakataji wa data yake, kuomba kuzuiwa kwa uchakataji wa data yake, au kuwasilisha malalamiko kwa Mchunguzi wa Umma wa Ulinzi wa Data wa Ufini kwa mujibu wa sheria ya ulinzi wa data inayotumika nchini Ufini. Haki ya mwenye data ya kufikia data yake ya kibinafsi inaweza kuwekewa vikwazo ikihitajika ili kuhakikisha uwezekano wa kuthibitisha ukweli wa ripoti hiyo au kulinda utambulisho wa mtumaji ripoti. Mwenye data ana haki ya kufahamishwa sababu za kizuizi na kuomba data ifichuliwe kwa Mpatanishi wa Ulinzi wa Data kwa mujibu wa sheria ya ulinzi wa data ya Ufini.

## Mdhibiti wa data na mchakataji data

Mdhibiti wa data ni Finnish Fund for Industrial Cooperation Ltd (Teollisen yhteistyön rahasto Oy), Kitambulisho cha Biashara 0356880-6, Porkkalankatu 22 A, 00180 Helsinki, Ufini. Mdhibiti anawajibikia data ya kibinafsi iliyochakatwa katika mfumo wa kuripoti malalamiko. Uchakataji wa ripoti kwa mujibu wa miongozo hii unatokana na wajibu wa kisheria wa Finnfund na maslahi halali kama mdhibiti wa data ili kuzuia hatari za kuharibu sifa, na ili kuunga mkono kanuni za maadili za biashara.

Mchakataji data ni WhistleB, Whistleblowing Center Ab (World Trade Center, Klarabergsvyadukten 70, SE-107 24 Stockholm, Uswidi). Mchakataji data anawajibikia utoaji wa huduma ya njia ya kutuma malalamiko, ikijumuisha kuchakata data iliyosimbwa kwa njia fiche kama vile ujumbe unaokusudiwa kufichua utovu wa nidhamu. WhistleB au wakandarasi wake wadogo hawawezi kusimbua na kusoma ujumbe uliosimbwa.

Uchakataji wa data ya kibinafsi inayohusiana na ufichuzi umefafanuliwa kwa kina zaidi katika sera ya faragha ya mfumo wa kutuma malalamiko wa Finnfund, ambayo inaweza kupatikana hapa: Finnfund Whistleblowing privacy policy (pdf, kwa Kiingereza au Kifini).

## Kuhamisha data nje ya EU na EEA

Data itahifadhiwa ndani ya Umoja wa Ulaya (EU). Kuhamisha data ya kibinafsi nje ya EU na Eneo la Kiuchumi la Ulaya (EEA) kwa ujumla hakuruhusiwi, isipokuwa hatua mahususi zichukuliwe ili kulinda uhamishaji wa data kwa mujibu wa kanuni halali na miongozo inayoidhinishwa kwa sasa.

## Taarifa zaidi:

- Mifumo ya kuripoti ya Finnfund
- Anwani nyingine (fomu ya mawasiliano)
- Maelezo ya mawasiliano
- Kwa vyombo vya habari
- Tuma ujumbe
- Ripoti kuhusu utovu wa nidhamu unaoshukiwa kutokea